

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI

MATOKEO YA MTIHANI WA DARASA LA SABA MWAKA 2022

Mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2022 ulifanyika tarehe 5 na 6 octoba 2022 nchini kote, katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, jumla ya shule 147 kati yake shule 138 za Serikali na shule 9 za watu binafsi na mashirika ya dini zilishiriki katika mtihani huo.

Jumla ya watahiniwa wapatao 13,295 walisajiliwa kati yako wavulana 6179 na wasichana 7116 ambapo jumla ya wanafunzi 13014 (97.89) kati yo wavulana 6020 (46.25) na wasichana 6994 (53.74 walifanya mtihani huo.

Katika matokeo hayo jumla ya wanafunzi 8456 sawa (65%) kati yao wavulana 3947 (46.67) na wasichana 4509 = 53.32% wamefaulu na kuchaguliwa kujiunga na Sekondari hapa chini.

Shule ya Mchepuo wa **Kiingereza ya Splendid Star** iliongoza katika matokeo hayo ikiwa na jumla ya wanafunzi 18 kati yao wavulana 8 na wasichana 10, ambao wote walipata ushindi wa daraja A ikiwa na wastani wa alama **285.55** ikifuatiwa na shule pia ya mchepuo wa Kiingereza ya Exodus iliyopata ushindi wa wastani wa alama **281.44**.

Shule ya Serikali ya Kigongo ilikuwa ni moja ya shule Bora Ki-wilaya ikiwa na wastani wa alama 207.01 ambayo ilikuwa na watahiniwa 152 kati yao wavulana 80 na wavulana 72 na waliofaulu ni 149 (98.02) kati yao wavulana 78 na wasichana 71 ikifuatiwa na shule ya Msingi Igokelo iliyopata wastani wa alama 191.27 ikiwa na watahiniwa wapatao 70 (95.9 %) kati yao wavulana 38 na wasichana 32.

Wanafunzi wenye mahitaji maalum kutoka shule ya Mitindo na baadhi ya shule pia wameonesha ufaulu wa hali ya juu sana jumla ya watahiniwa wapatao 76 kati yao wavulana 37 na wasichana 39 walifanya mtihani huo, waliochaguliwa kujiunga na sekondari ni wanafunzi 62 (81.57) ambapo mwanafunzi **Benedict James kapelega** kutoka shule ya Rishor iliyoko kata ya Idetemya alipata wastani wa alama A. kwa kila somo.

Shule ambazo zimeonesha ushindi duni katika mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi Mwaka 2022 ni pamoja na Shule ya Msingi Nyashitanda kata ya Shilalo iliyokuwa na jumla ya watahiniwa 55 kati yao wavulana 25 na wasichana 30 ilipata wastani wa alama 88.78, katika ushindi huo, jumla ya wanafunzi 4 kati yao wavulana 2 na wasichana 2 ndiyo waliochaguliwa kujiunga na masomo ya Sekondari.

Ushindi huu kwa Wilaya ya Misungwi ni ushindi wa **wastani** ambao kimsingi umetokana na ushirikiano baina ya ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mh Veronica Kessy. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, Ofisi ya Elimu Msingi Misungwi na wadau wote wa Elimu Misungwi, hususani walimu, Maafisa Elimu kata na Watendaji wa kata na vijiji.

Misungwi tunaamini kuwa uendeshaji na usimamizi makini wa mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi ndiyo silaha pekee itakayoendelea kuboresha, kuinua na kuleta ushindi wa haki miongoni mwa watahiniwa wa mitihani ya kitaifa.

Pamoja na ushindi huo, zipo changamoto kadhaa ambazo zinatakiwa kupunguzwa au kuondolewa kabisa, changamoto hizo ni pamoja na :-

- i) Utoaji wa chakula cha mchana kwa wanafunzi wote katika shule za msingi. Hii itatokana na kuendelea kuelimisha jamii juu ya wazazi/walezi kuhamisha chakula cha watoto wao, hasa wakati wa mchana kwa kupeleka chakula chao shuleni.
- ii) Uongezaji wa Miundo mbinu ya vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na nyumba za walimu. Jamii ielezwe waziwazi juu ya umuhimu wa uwepo wa miundo mbinu hiyo shuleni kwa kushirikiana na Serikali.
- iii) Kuweka nguvu kubwa ya ufundishaji kwa madarasa ya Awali hadi darasa la pili, ili wanafunzi wote wanaosajiliwa darasa la tatu wawe na ufahamu wa stadi za kuandika, kuhesabu na kusoma.
- iii) Kuendelea kuboresha na kutoa stahiki na maslahi ya walimu kwa wakati ili kuongeza Ari ya ufundishaji shuleni, sambamba na mikakati ya kuongeza na kuboresha utoaji wa motisha kwa walimu, wanafunzi, wadau wa elimu na jamii zinazojitolea katika uboreshaji wa ufundishaji na ujifunzaji.
- iv) **Baadhi ya wazazi kuwaficha wanafunzi wenye ulemavu** jamii ihamasishwe na ielimishwe juu ya umuhimu wa kuwapeleka shule kwa hiari muda wa kuandikisha unapofika kwa wanafunzi wenye ulemavu; kwani kuwapa elimu ni kuwapunguzia au kuwaondolea kabisa hali ya utegemezi usio wa lazima ili waweze kujimudu na kujitegemea katika Mazingira yao.

Mwisho: Shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayongozwa na Mh. Dr. Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuboresha Mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga Miundo mbinu, ununuzi wa vitabu na utoaji wa ajira kwa walimu pamoja na kuboresha Maslahi yao.

Moto wetu ni **“Misungwi ni yetu tushirikiane kujenga”**


Benson P. Mihayo

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

MISUNGWI

**VIKURUGENZI MTENDAJI
KALIMASHAURI YA WILAYA
MISUNGWI**